# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS

# TUME YA UTUMISHI WA UMMA

## CHANGAMOTO ZA TUME INAVYOFANYA KAZI KAMA TUME REKEBU

**Mada iliyotolewa katika Mkutano (Retreat) wa Tume utakaofanyika tarehe 23 – 25/07/2009 katika Ukumbi wa Hotel ya Morogoro,**

## YALIYOMO:

1.0 UTANGULIZI

2.0 DHANA YA TUME KUWA REKEBU

3.0 MAJUKUMU YA TUME KWA MUJIBU WA MAREKEBISHO YA SHERIA NA.18 YA MWAKA 2007

4.0 KAZI ZA TUME REKEBU

5.0 HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUTOKANA NA TAARIFA ZA UKAGUZI WA RASILIMALI WATU

6.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME

## 1:0 UTANGULIZI:

Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kwa kutunga Sheria Na. 18 ya mwaka 2007. Marekebisho hayo yameondoa Tume kuwa TENDAJI na kuwa Tume REKEBU.

Lengo la mada hii ni kujadili namna ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili Tume katika kutekeleza jukumu lake la urekebu katika kusimamia uendeshaji wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

***Inaendelea……***

## 2.0 DHANA YA TUME KUWA REKEBU

Dhana ya Tume kuwa REKEBU siyo ngeni katika utendaji wa shughuli za Serikali, imekuwepo kwa kusudio la kusimamia vyema utekelezaji wa Sheria mbalimbali za Nchi. Hapa nchini Tanzania ipo mifano ya Taasisi za Serikali ambazo zimekuwa zikifanya kazi za UREKEBU ili kuhakikisha kuwa vyombo mbalimbali kwenye sekta ya Umma na binafsi vinatoa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Vyombo hivyo ni kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS), SUMATRA, EWURA, Mamlaka ya Chakula na Madawa (TFDA), ni baadhi ya vyombo vya UREKEBU.

## 3.0 MAJUKUMU YA TUME KWA MUJIBU WA MAREKEBISHO YA SHERIA NA.18 YA MWAKA 2007

Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya Mwaka 2007 katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002 kimerekebishwa kwa kufuta Aya (c) na (d) na badala yake kuweka Aya (c) yenye maneno yafuatayo "**to issue guidance and monitor compliance in the Service".** Vifungu hivi vilitoa Tume kwenye Sura Tendaji na kubakia Rekebu. Hata hivyo Tume itaendelea na majukumu yake yaliyoko katika Kifungu Na.10(1)

Majukumu ya msingi ni pamoja na:-

- Kumshauri Mheshimiwa Rais kama atakavyohitaji hususani ujazaji wa nafasi wazi katika Utumishi wa Umma.
- Kupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko
- Kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji katika Utumishi wa Umma.

*Inaendelea……..*

## 3.1 Majukumu ya Idara ya Utumishi wa Walimu

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) Idara ya Utumishi wa Walimu itaendelea kutekeleza majukumu ya KIUTENDAJI ya kuwa Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu. Idara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuajiri walimu
- Kusajili walimu
- Kuthibitisha kazini na kuwapandisha vyeo walimu
- Kushughulikia masuala ya nidhamu
- Mirathi na Pensheni.

Idara ya Utumishi wa walimu haikuguswa na marekebisho yaliyofanywa imebakia na majukumu yake yaliyoko kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002.

## 4.0 KAZI ZA TUME REKEBU

Katika kutekeleza suala la usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma, Tume inatekeleza kazi zifuatazo:-

## 4.1 Kuandaa na kusambaza Miongozo na maelekezo. (kuwa na mfumo mmoja wa usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma)

1. Mwongozo wa ajira.
2. Mwongozo wa nidhamu na rufaa.
3. Maelekezo mahsusi kwa Mamlaka za nidhamu na Kamati za uchunguzi kuhusu namna ya kuendesha uchunguzi wa mashauri ya nidhamu Na. 1 ya mwaka 2008.

*Inaendelea……..*

## 4.2 Kuweka Viwango vya uzingatiaji wa Sheria. **(viwango vitakavyotumika kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa)**

Mfumo wa Tume umeweka viwango vya uzingatiaji.

1. Kiwango cha juu (75 – 100%)
2. Kiwango cha Kati (50 – 74%)
3. Kiwango cha chini (25 – 49%)
4. Kiwango hafifu (0 – 24%)

## 4.3 Kuwezesha. (**uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Usimamizi wa Rasilimali watu)**

1. Kupitia Radio na magazeti.
2. Vipeperushi.
3. Mikutano ya wadau.
4. Semina.
5. Ziara.

*Inaendelea ....*

## 4.4 Kufuatilia taarifa za utekelezaji usimamizi wa Rasilimali watu.


Taarifa hizo zinawasilishwa Tume kwa mujibu :-

**1. Mwongozo wa kuwasilisha taarifa Tume**

Taasisi zilizowasilisha taarifa kwa kipindi cha robo mwaka tatu katika mwaka wa fedha 2008/09.

| Na. | Taasisi | Idadi | Taasisi zilizowasilisha | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Robo ya kwanza | Robo ya pili | Robo ya tatu |
| 1. | Wizara | 25 | 5 | 3 | 9 |
| 2. | Sekretarieti za Mikoa | 21 | 12 | 9 | 9 |
| 3. | Idara zinazojitegemea | 15 | 5 | 5 | 6 |
| 4. | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 133 | 22 | 36 | 41 |
| | **Jumla** | **194** | **44** | **53** | **65** |

*Inaendelea ……*




Chati inaonyesha kuwa katika robo ya tatu Taasisi zisizowasilisha zilikuwa zaidi ya nusu, robo ya kwanza asilimia **77,** robo ya pili asilimia **73,** na robo ya tatu asilimia **66.**

2. **Waraka wa Tume Kumb. Na. PSC/CAB/117/355/01/6 ya tarehe 11/12/2008, kuhusu Ajira katika Utumishi wa Umma baada ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi Kumb. Na. C/AC.45/257/01/C/99 na tarehe 12/5/2008.**

Utekelezaji wa Waraka huo wa Tume hadi Mei, 2009 Taasisi zilizowasilisha ni:

***Inaendelea ……***

| Na. | Taasisi kisekta | Idadi ya Taasisi | Taasisi zilizowasilisha |
|---|---|---|---|
| 1. | Wizara | 25 | 2 |
| 2. | Sekretarieti za Mikoa | 21 | 6 |
| 3. | Idara zinazojitegemea | 15 | 2 |
| 4. | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 133 | 3 |
| | Jumla | 194 | 13 |

*Inaendelea….*

Jedwali linaonyesha kuwa ni Taasisi **13** zilizowasilisha kati ya Taasisi **194**, utekelezaji wa masuala ya ajira, upandishwaji vyeo na kuthibitishwa kazini.

Taarifa hizi hazitoi hali halisi ya utekezaji wa masuala yaliyotekelezwa na Mamlaka za Ajira kwa  kipindi husika.

***Inaendelea….***

## 4.5 Kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

Kufuatia Taarifa za utekelezaji zinazowasilishwa Tume na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu au Malalamiko yanayowasilishwa na watumishi wa Umma, Tume huchukua hatua zifuatazo:-

i.) **Ukaguzi wa kawaida.**

Ukaguzi huu hufanyika kwa kutumia "Mfumo wa Ukaguzi wa Rasilimali watu katika maeneo ya Ajira, Nidhamu, likizo ya kawaida, OPRAS na Likizo ya ugonjwa. (**Katika mwaka wa fedha 2008/09 hakuna Ukaguzi wa kawaida wa mfumo huo uliofanyika**).

*Inaendelea….*


## ii.) Ukaguzi maalum.

Ukaguzi huu hufanyika kwa kuzingatia Hadidu za Rejea zinazotolewa na Katibu wa Tume kuainisha Taarifa/malalamiko yaliyowasilishwa Tume. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2008/09 Tume imefanya kaguzi maalum zifuatazo:-

*Inaendelea…..*


| Na. | Taasisi zilizokaguliwa | Eneo | Taarifa/ Malalamiko |
|---|---|---|---|
| 1. | Idara ya Utumishi wa Walimu (Waajiri) katika Mkoa wa Mbeya, Pwani, Dara es salaam na Mwanza. | Upandishwaji vyeo. | UTUMISHI |
| 2. | Wizara ya Miundo mbinu | Upandishwaji vyeo. | Malalamiko (UTUMISHI) |
| 3. | Wizara ya Elimu | Upandishwaji vyeo. | Malalamiko (TUME) |
| 4. | Wizara ya kazi, ajira na maendeleo ya vijana | Upandishwaji vyeo. | Malalamiko (TUME) |
| 5. | Wizara ya Kilimo na chakula | Upandishwaji vyeo. | Taarifa ya utekelezaji |

# TUME INAVYOSIMAMIA RASILIMALI WATU KATIKA UTUMISHI WA UMMA



# 5.0 HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUTOKANA NA TAARIFA ZA UKAGUZI WA RASILIMALI WATU.

Katibu wa Tume huwasilisha taarifa ya ukaguzi kwenye Tume kwa ajili ya uamuzi kama inavyoonyesha kwenye mchoro.



KATIBU MKUU KIONGOZI
OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
MAAGIZO
MAPENDEKEZO /USHAURI
KATIBU (SEKRETARIETI)
MATOKEO YA UKAGUZI
TUME (Uamuzi)
MAAGIZO
MAELEKEZO (MREJESHO)
MAAGIZO
MAAGIZO
WAAJIRI, MAMLAKA ZA AJIRA NA NIDHAMU

1. **Tume hutoa (feedback) mrejesho kwa Taasisi zilizokaguliwa na maelekezo ya namna ya kuboresha usimamizi wa Rasilimali watu. (Taasisi zilizokaguliwa hupelekewa taarifa za ukaguzi).**

   Maamuzi yaliyofanywa na Tume kufuatia Taarifa za Ukaguzi ni pamoja na:-

- Kukasimu madaraka ya kushughulikia masuala ya Ajira na Nidhamu kwa walimu kwa Kamati za Wilaya na Kamati za Mikoa.
- Kukasimu madaraka ya kuwaandikia barua za kupandishwa vyeo walimu kwa Waajiri wao.
- Maelekezo mahsusi kwa Mamalaka za Nidhamu na Kamati za Uchunguzi kuhusu namna ya kuendesha uchunguzi wa Mashauri ya Nidhamu Na.1 ya mwaka 2008.

*Inaendelea…..*

- Waraka kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wa kuwachukulia watumishi hatua za nidhamu wa tarehe 27 Agosti, 2008.
- Waraka kuhusu mapungufu yanayojitokeza katika kushughulikia mashauri ya Nidhamu wa tarehe 27 Februari, 2007.
- Waraka kuhusu wajumbe wa Tume ya Utumishi wa umma katika Kamati/Kamati maalum /Bodi za Ajira wa tarehe 1 Septemba, 2006
- Waraka kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ajira wakati wa kuajiri wa tarehe 12 Agosti, 2005.

2. **Tume hutoa mapendekezo na ushauri kwa Mkuu wa Utumishi wa Umma (Katibu Mkuu Kiongozi) au Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, hatua za kuchukua kwa Taasisi ili kuondoa upungufu ulioainishwa kwenye kaguzi hizo.**

   Mfano mmojawapo wa hatua ambazo zimeweza kuchukuliwa ni marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002 kuiondoa Tume kushiriki katika mchakato wa ajira.

## 6:0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME.

Tume katika kutekeleza jukumu lake la urekebu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Tume kuwa na Mamlaka ya kutengua au kutoa maagizo pale masuala ya ajira na nidhamu yanapokiukwa.
- Kuwa na Mifumo itakayorahisisha ufuatiliaji wa Taarifa za Utekelezaji wa usimamizi wa Rasilimali watu kutoka kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu

- Kuwa na Mfumo wa ukaguzi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma utakaowezesha Tume kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Rasilimali watu kwa kuzingatia Taratibu za uendeshaji wa makundi yaliyo katika Utumishi wa Umma.

- Kuwa na Mifumo itakayowezesha Tume kuwa na “Database” ya Takwimu za watumishi wa Umma.

- Idara ya Utumishi wa Walimu katika Tume kufanya kazi za UREKEBU kama Idara zingine na si kuwa TENDAJI kwa maana ya kuwa Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu katika Utumishi wa Umma

- Mkutano huu hujadili namna ya kukabiliana  na changamoto hizi zinazoikabili Tume ili kuwezesha kuwa na Mifumo imara itakayowezesha kutekeleza majukumu ya Tume kwa ufanisi.

## 7:0 MWELEKEO (THE WAYFORWARD).

Ni matarajio ya Tume kuwa baada ya mkutano huu tutajenga misingi itakayotuwezesha kuwa na mifumo imara ya itakayowezesha Tume kutekeleza majukumu yake yote kwa wakati na ufanisi.

## 8:0 HITIMISHO

Mada hii imejadili kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 10(1) hususan kuhusiana na jukumu la UREKEBU. Tume itapaswa kujizatiti ili kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi ili kuiewezesha Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi.

# ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

***IMETOLEWA NA*:**

**Bibi THECLA W.   SHANGALI,**

**KATIBU,**

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA,**

**S.L.P. 9143,**

**DAR ES SALAAAM.**